

Karibuni katika

VIWANGO VYA USTADI VINAMAANISHA NINI?

Kwa kutegemea alama ambazo mtoto wako atapata, anaweza kuzingatiwa kama yeye ni ELL/MLL. Maelezo ya viwango vya ustadi yametolewa hapa chini:

Kiwango	Maelezo ya Ustadi wa Lugha ya Kiingereza	Wanaostahili Kupata Huduma
Kuingia (Kiwango cha Kuanzia)	Mwanafunzi katika kiwango cha Kuingia ana utegemezi mkubwa katika misaada na miundo ya kuendelea katika stadi za lugha kitaaluma na bado hajafikia kiwango kinachohitaji katika kuonesha ustadi wa lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya kitaaluma.	
Kuchipukia (Kiwango cha Kati, Chini)	Mwanafunzi katika kiwango cha Kuchipukia ana utegemezi fulani katika misaada na miundo ya kuendelea katika stadi za lugha kitaaluma na bado hajafikia kiwango kinachohitajika katika kuonesha ustadi wa lugha ya Kiingereza katika mazingira kadhaa ya	Wanaostahili Kupata Huduma

Kiwango	Daraja ya K-8 Dakika za Kusomeshwa ENL kwa Wiki	Daraja ya 9-12 Dakika za Kusomeshwa ENL kwa Wiki	Wanafunzi katika Programu za Lugha Mbili
Kuingia (Kiwango cha Kuanzia)	Dakika 360	Dakika 540	Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani Kiwango cha chini cha maudhui ya masomo 2 katika lugha mbili
Kuchipukia (Kiwango cha Kati, Chini)	Dakika 360	Dakika 360	Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani Kiwango cha chini cha maudhui ya masomo 2 katika lugha mbili
Kipindi cha Mpito (Kiwango cha Kati)	Dakika 180	Dakika 180	Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani Kiwango cha chini cha maudhui ya somo 1 katika lugha mbili
Kupanuka (Kiwango cha Juu)	Dakika 80	Dakika 180	Mwendo 1 ya Sanaa ya Lugha Nyumbani Kiwango cha chini cha maudhui ya somo 1 katika lugha mbili

MARA NIPATAPO MATOKEO, VIPI NINaweza KUSAIDIA NYUMBANI?

Msomee mtoto wako katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani na / au katika lugha ya Kiingereza (utafiti unaonyesha kuwa kumsomea mtoto wako katika lugha yake ya nyumbani itamsaidia katika ujuzi wa kusoma na kuandika Kiingereza).

Mtolee hadithi mtoto wako katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani.

Tembelea maktaba ya eneo lako na azima vitabu vya kielektroniki vya kusikiliza vilivyo katika lugha yake ya msingi au ya nyumbani au Kiingereza.

Hakikisha unahudhuria mikutano ya walimu na wazazi inayopangwa na shule ya mtoto wako.

Panga mkutano binafsi na mwalimu wa mtoto wako ili kujifunza njia maalumu ambazo unaweza kumsaidia mtoto wako kufanikiwa.

Panga wakati kila siku kwa mtoto wako wa kufanya kazi za nyumbani na ikiwezekana, mtafutie pahali penye utulivu, pasipo na usumbufu, ambapo anaweza kufanya kazi.

Andaa matembezi ya kifamilia katika makumbusho. Miongozo katika makumbusho yanaweza kukusaidia kutembelea maonyesho pamoja na mtoto wako.

Makumbusho na maktaba mara nyingi hutoa ofa za gharama nafuu/au bure wakati wa baada ya shule au wikiendi.

Kwa ajili ya maswali au mashaka kuhusu huduma za ELL tafadhali wasiliana na:
nysparenthotline@nyu.edu
Nambari ya Simu ya ELL kwa Mzazi: (800) 469-8224

maswali Zingine?

Tafadhali tuma maswali au maoni yako kwa Ofisi ya Elimu kwa
Lugha Mbili na Lugha za Dunia OBEFLS@nysed.gov

Kwa maelezo zaidi juu ya NYSITELL tembelea tovuti hii:
<http://www.p12.nysed.gov/assessment/nysitell/>

